

**Mamlaka ya Mawasiliano  
Tanzania**

# **Ripoti ya Sekta ya Mawasiliano**

**Robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024**

**[www.tcra.go.tz](http://www.tcra.go.tz)**

**VIWANGO VYA ISO 9001: 2015**

**Toleo 1.0**

## **Kuhusu ripoti hii**

Ripoti hii inawasilisha takwimu za mawasiliano za robo ya pili ya mwaka wa fedha 2024/2025. Kwa ujumla, ripoti inatoa takwimu za mawasiliano ya simu, pesa mtandao, Intaneti, utangazaji, posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto.

Takwimu zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU) vya kukusanya na kuandaa takwimu za huduma ya mawasiliano/TEHAMA.

---

# Yaliyomo

<b>1</b>	<b>Huduma ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti</b>	<b>1</b>
1.1	Idadi ya laini za simu	2
1.2	Bei za huduma ya mawasiliano ya simu	6
1.3	Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS kwa huduma ya mawasiliano ya simu)	10
1.4	Kuzuru	15
1.5	Vifaa vya Mawasiliano vinavyotumia laini za simu	16
1.6	Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu	17
1.7	Mgawanyo waa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu	18
1.8	Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano	19
1.9	Huduma za intaneti	20
1.10	Huduma za pesa mtandao	25
1.11	Ubora wa huduma za simu na Intaneti	27
1.12	Majaribio ya ulaghai	35
1.13	Leseni za mawasiliano ya simu na Intaneti	38
1.14	Vyeti	38
<b>2</b>	<b>Huduma ya Utangazaji</b>	<b>40</b>
2.1	Visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu	40
2.2	Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya	41
2.3	Ueneaji wa huduma ya utangazaji	43
2.4	Utekelezaji wa masharti ya leseni ya utangazaji	43
2.5	Leseni za utangazaji	46
<b>3</b>	<b>Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto</b>	<b>48</b>
3.1	Idadi ya masanduku ya posta	48
3.2	Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto	48
3.3	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa	48
3.4	Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelekwa	50
3.5	Ubora wa huduma za Posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto	51
3.6	Leseni za huduma ya Posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto	52
<b>4</b>	<b>Hitimisho</b>	<b>53</b>


# Muhtasari wa takwimu za Sekta ya Mawasiliano



Idadi ya laini za simu

**86.8 M**

Utumiaji wa intaneti



**48.0 M**

Upenyu

**42.5 B**

Idadi ya dakika kutoka nje ya nchi

**617 PB**



Idadi ya dakika ndani ya nchi




**37.3 M**



Matumizi ya intaneti

Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa

**2.1 M**



**16.8 K**

Televisheni kwa njia ya waya

Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya intaneti ya kasi

**91%**

3G

**20%**



4G

**88%**

Simu Janja

**472,216**

Bidhaa zilizotumwa


**63,994**




**480,757**

Bidhaa zilizopokelewa

**93,527**



Upenyu



**23 M**

# Sura ya kwanza

## Huduma ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti



# 1. Huduma ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti

Sehemu hii inawasilisha takwimu za laini ya simu, bei, idadi ya dakika, ujumbe mfupi wa maneno (SMS), huduma ya intaneti, miundombinu na vifaa vya mawasiliano, upatikanaji wa huduma, ubora wa huduma na idadi ya watoa huduma.

## 1.1. Idadi ya laini za simu

Sehemu hii inawasilisha idadi ya laini za simu za mkononi na za mezani ambazo zilitumika kwenye huduma ya mawasiliano angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Kuna aina mbili za laini: zinazotumika kwa mawasiliano ya binadamu (Person to Person - P2P) na zinazotumika kwa mawasiliano ya vifaa na mitambo (Machine to Machine - M2M).

Jumla ya idadi ya laini (P2P na M2M) zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka milioni 80.7 katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 hadi milioni 86.8 kwa robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024, hilo ni ongezeko la asilimia 7.7 kama inavyoonekana hapo chini.

Kufikia Septemba 2024

Kufikia Disemba 2024

**Milioni 80.7**

**Milioni 86.8**

**7.7%**



Jedwali 1.1 linaonesha idadi ya laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa kwa kipindi kinachoishia Disemba 2024.

### Jedwali 1.1 Idadi ya laini za simu za mkononi (P2P na M2M) na mezani

Mwezi	Simu za mkononi	Simu za mezani	Jumla
Oktoba	81,937,425	78,134	82,015,559
Novemba	84,253,866	78,513	84,332,379
Disemba	86,769,161	78,299	86,847,460

#### 1.1.1 Idadi ya laini za P2P

##### Kielelezo 1.1.1 Idadi ya laini za P2P



Mpaka kufikia Disemba 2024

**Milioni 85.8**

**Milioni 79.6**

Mpaka kufikia Septemba 2024

**7.8%**

Laini za simu za mkononi na mezani zilizosajiliwa kwa ajili ya P2P zimeongezeka kwa takribani milioni 7.8 katika robo mwaka inayoishia Disemba 2024

## Jedwali 1.1.1 Idadi ya laini za simu za P2P zilizosajiliwa kwa kila mtoa huduma

Mwezi	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Jumla
Oktoba	19,592,918	11,340,364	24,082,694	1,601,775	24,416,163	81,033,914
Novemba	19,835,221	11,779,672	24,716,983	1,621,942	25,323,277	83,277,095
Disemba	20,061,071	12,371,713	25,419,851	1,655,861	26,327,611	85,836,107

## 1.1.2 Idadi ya laini za simu kwa ajili ya vifaa (M2M)

### Kielelezo 1.1.2 Idadi ya laini za M2M

Laini zilizosajiliwa kwa ajili ya mawasiliano ya M2M zimepungua kwa laini 4,467 kwa robo mwaka iliyoishia Disemba 2024.

Mpaka kufikia Disemba 2024

**Milioni 1.01**

0.4% ↓

**Milioni 1.02**

Mpaka kufikia Septemba 2024



Jedwali 1.12 linaonesha idadi ya laini za simu kwa ajili ya matumizi ya vifaa kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Disemba 2024

### Jedwali 1.1.2 Idadi ya laini za M2M zilizosajiliwa


Mwezi	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Jumla
Oktoba	335,891	60,903	46,521	4,501	533,829	981,645
Novemba	339,039	71,709	47,435	4,501	546,079	1,008,763
Disemba	339,301	73,059	48,870	4,450	545,673	1,011,353

## 1.1.3 Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma


Chati 1.1.3a na 1.1.3b zinaonesha mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma. Takwimu za P2P kwa ujumla zinaonesha kuna ushindani mkubwa kati ya watoa huduma.

Katika usajili wa M2M, Vodacom inaongoza ikiwa na 54.0% ya laini zote zilizosajiliwa. Airtel inashika nafasi ya pili kwa 33.5%, ikifuatiwa na Halotel kwa 7.2%. Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma ni kama unavyoonekana kwenye Chati 1.1.3b.

**Chati 1.1.3a Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa P2P**



**Chati 1.1.3b Mgawanyo wa laini za simu kwa kila mtoa huduma wa M2M**



### 1.1.4 Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa na jinsia

**Kielelezo 1.1.4 Idadi ya laini za simu kwa kila jinsia**




**44,639,594**  
**51.4%**

**42,207,866**  
**48.6%**



Idadi ya laini za simu kwa kila mkoa imeoneshwa kwenye ramani 1.1.4. Katika robo ya pili ya mwaka 2024/2025. Dar es Salaam ilishika nafasi ya kwanza kwa kuwa na laini milioni 15.98, Mwanza ilishika nafasi ya pili kwa kuwa na laini milioni 5.75, Arusha ilishika nafasi ya tatu kwa kuwa na laini milioni 5.23, Mbeya ilishika nafasi ya nne ikiwa na laini milioni 4.99, na Dodoma ilishika nafasi ya tano kwa kuwa na laini milioni 4.64.

### Ramani 1.1.4 Idadi ya laini za simu za mkononi na mezani kwa kila mkoa



### 1.1.5 Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa kipindi cha robo mwaka

Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa ajili ya mawasiliano ya simu kwa robo mwaka na kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita imeoneshwa katika Jedwali 1.1.5a na 1.1.5b

**Jedwali 1.1.5a Mwenendo wa idadi ya laini za simu kwa kipindi cha robo mwaka**

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
Laini za simu za mkononi	72,418,634	76,535,958	80,583,993	86,769,161
Laini za simu za mezani	77,461	80,164	78,048	78,299
<b>Jumla</b>	<b>72,496,095</b>	<b>76,616,122</b>	<b>80,662,041</b>	<b>86,847,460</b>
<b>Asilimia ya Ueneaji</b>	<b>112%</b>	<b>116%</b>	<b>124%</b>	<b>133%</b>

## Jedwali 1.1.5b Idadi ya laini za simu kwa miaka mitano iliyopita

	2020	2021	2022	2023	2024
Simu za mkononi	51,220,233	54,044,384	60,192,331	70,215,144	86,769,161
Simu za mezani	72,469	71,834	84,696	75,732	78,299
<b>Jumla</b>	<b>51,292,702</b>	<b>54,118,218</b>	<b>60,277,027</b>	<b>70,290,876</b>	<b>86,847,460</b>
<b>Asilimia ya Ueneaji</b>	<b>81%</b>	<b>88%</b>	<b>98%</b>	<b>111%</b>	<b>133%</b>





## 1.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu

Sehemu hii inawasilisha wastani wa bei nje ya vifurushi na ndani ya vifurushi (pamoja na kodi) kwa huduma za sauti, SMS, na data kwa matumizi ya ndani na nje ya mtandao, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

### 1.2.1 Bei za huduma za mawasiliano ya simu nje ya kifurushi

Hizi ni bei zinazotowazwa kwa huduma za sauti, SMS, na data.

#### Kielelezo 1.2.1 Bei za huduma za mawasiliano ya simu

	Septemba 2024	Disemba 2024	Mabadiliko (%)
Ndani ya mtandao 	26.00	26.00	0%
Nje ya mtandao	28.00	28.00	0%
SMS Kitaifa 	7.80	7.80	0%
SMS Kimataifa	189.61	189.61	0%
Afrika Mashariki 	696.68	597.40	-14.3%
Mataifa mengine	1,948.22	2,016.70	3.5%
Data 	9.35	9.35	0%

Kama inavyooneshwa katika muhtasari hapo juu, wakati bei za kupiga simu ndani na nje ya mtandao, SMS kitaifa (local SMS), SMS kimataifa na data hazikubadilika, bei za kupiga simu za Afrika Mashariki zilipungua kwa 14.3% na mataifa mengine ziliongezeka kwa 3.5%.

### 1.2.1.1 Bei za huduma ya sauti (Tsh)

Bei za huduma ya sauti kwa robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024 kwa simu za ndani na nje ya nchi zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1.1 Hizi ni bei za sauti kwa dakika moja kwa kupiga simu ya ndani au ya kimataifa bila kujiunga kwenye kifurushi.

#### Jedwali 1.2.1.1 Bei (Tsh) za kupiga simu ndani na nje ya nchi kwa kila mtoa huduma

Mtoa huduma	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	Afrika Mashariki	Mataifa mengine
Airtel	30.00	30.00	614.40	1,426.60
Halotel	10.00	20.00	875.00	1,565.00
Yas	30.00	30.00	1,030.00	1,673.33
TTCL	30.00	30.00	217.60	2,871.33
Vodacom	30.00	30.00	250.00	2,547.22
<b>Wastani</b>	<b>26.00</b>	<b>28.00</b>	<b>597.40</b>	<b>2,016.70</b>

Jedwali 1.2.1.1 linaonesha kuwa watoa huduma wote walitoza Tsh 30 kwa dakika ndani na nje ya mtandao, isipokuwa Halotel alitoza Tsh 10 kwa dakika ndani ya mtandao na Tsh 20 nje ya mtandao. Wastani wa bei ya huduma ya sauti ndani ya mtandao katika robo mwaka inayoishia Disemba 2024 ilibaki sawa na robo mwaka iliyoishia Septemba 2024.

Aidha, Jedwali 1.2.1.1 linaonesha kuwa bei ya huduma ya sauti kimataifa zilitofautiana baina ya watoa huduma. Wastani wa bei ya huduma ya sauti kwa dakika moja kwa Afrika Mashariki na nchi nyingine ni Tsh 597.40 na 2,016.70 mtawalia.

### 1.2.1.2 Bei za SMS na data (Tsh)

Bei bila kifurushi nje na ndani ya nchi kwa SMS na data hadi Disemba 2024 zimeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.1.2

#### Jedwali 1.2.1.2 Bei (Tsh) za SMS na data

Mtoa huduma	SMS ndani ya nchi	SMS nje ya nchi	Data/Mb
Airtel	8.00	215.00	9.35
Halotel	5.00	95.00	9.35
Yas	8.00	215.00	9.35
TTCL	10.00	138.06	9.35
Vodacom	8.00	285.00	9.35
<b>Wastani</b>	<b>7.80</b>	<b>189.61</b>	<b>9.35</b>

Wastani wa bei za SMS kitaifa (Tsh 7.80), SMS nje ya nchi (Tsh 189.61) na data (Tsh 9.35) kwa Disemba 2024 ulibaki kama ilivyokuwa kwenye robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024.

## 1.2.2 Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa dakika moja ya sauti, SMS moja na MB moja ya data kwa watumiaji waliojiunga na kifurushi zimeoneshwa kwenye jedwali 1.2.2a

### Jedwali 1.2.2a Mabadiliko ya bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Kipindi	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Julai- Sept 2024	4.75	6.34	1.47	2.17
Okt- Dis 2024	4.79	6.27	1.57	2.16
<b>Badiliko %</b>	<b>0.82%</b>	<b>-1.04%</b>	<b>10%</b>	<b>-0.61%</b>

Jedwali 1.2.2a linaonesha kuwa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi zimebadilika katika robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024 ikilinganishwa na robo ya mwaka inayoishia Septemba 2024. Bei za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao, na SMS ziliongezeka kwa viwango tofauti kama ilivyooneshwa.

Jedwali 1.2.2b linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu katika kifurushi ziko chini ikilinganishwa na bei za huduma za mawasiliano ya simu bila kifurushi kama inavyooneshwa.

### Jedwali 1.2.2b Bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi

Mtoa huduma	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Airtel	4.39	7.82	1.68	2.05
Halotel	3.02	4.76	1.00	2.16
Yas	4.66	5.44	1.19	2.06
TTCL	7.33	7.33	2.28	2.26
Vodacom	4.55	6.03	1.71	2.27
<b>Wastani kwa Sekta</b>	<b>4.79</b>	<b>6.27</b>	<b>1.57</b>	<b>2.16</b>

## 1.2.3 Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu

Wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu ndani na nje ya kifurushi umeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.3.

### Jedwali 1.2.3 Wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu

	Ndani ya mtandao	Nje ya mtandao	SMS	Data
Wastani bila kifurushi	26.00	28.00	7.80	9.35
Wastani katika kifurushi	4.79	6.27	1.57	2.16

Jedwali 1.2.3 linaonesha kuwa wastani wa bei za huduma ya mawasiliano ya simu bila kifurushi ni karibu mara tano zaidi ya wastani wa bei katika kifurushi na hivyo kupelekea watumiaji wengi (99.9%) kupendelea kujiunga na huduma za vifurushi.

### 1.2.4 Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za mawasiliano ya simu

Mwenendo wa wastani wa bei za huduma za sauti na SMS nje ya vifurushi, kitaifa na kimataifa katika kipindi cha robo mwaka na miaka mitano umeoneshwa kwenye Jedwali 1.2.4a, 1.2.4b, 1.2.4c, 1.2.4d, 1.2.4e, 1.2.4f, 1.2.4g na 1.2.4h.

#### Jedwali 1.2.4a Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za sauti kitaifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
Ndani ya mtandao	26.00	26.00	26.00	26.00
Nje ya mtandao	28.00	28.00	28.00	28.00

#### Jedwali 1.2.4b Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za sauti kitaifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano

	2020	2021	2022	2023	2024
Ndani ya mtandao	57.00	34.00	32.00	29.00	26.00
Nje ya mtandao	57.00	34.00	32.00	30.00	28.00

#### Jedwali 1.2.4c Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za sauti kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
Afrika Mashariki	727.80	713.16	696.68	597.40
Mataifa mengine	1,899.00	1,869.45	1,948.22	2,016.70

#### Jedwali 1.2.4d Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za sauti kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano

	2020	2021	2022	2023	2024
Afrika Mashariki	830.00	966.00	1,103.00	1,171.00	684.00
Mataifa mengine	1,379.00	1,564.00	1,817.00	1,776.00	2,055.00

#### Jedwali 1.2.4e Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za kutuma SMS kitaifa na kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
SMS kitaifa	7.80	7.80	7.80	7.80
SMS kimataifa	189.60	189.60	189.60	189.61

#### Jedwali 1.2.4f Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za kutuma SMS kitaifa na kimataifa nje ya vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano

	2020	2021	2022	2023	2024
SMS kitaifa	20.00	13.00	11.00	11.00	7.80
SMS kimataifa	176.00	172.00	193.00	200.00	189.61

### Jedwali 1.2.4g Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
Ndani ya mtandao	4.50	4.66	4.75	4.79
Nje ya mtandao	6.07	6.18	6.34	6.27
SMS	1.37	1.42	1.47	1.57
Data	2.17	2.16	2.17	2.16

### Jedwali 1.2.4h Mwenendo wa wastani wa bei (Tsh) za huduma za mawasiliano ya simu katika vifurushi kwa kipindi cha miaka mitano

	2020	2021	2022	2023	2024
Ndani ya mtandao	9.38	7.84	7.27	4.90	4.68
Nje ya mtandao	11.21	8.69	7.78	6.30	6.22
SMS	3.45	3.35	2.69	1.37	1.46
Data	1.73	1.61	1.86	2.14	2.17

## 1.3 Idadi ya dakika na ujumbe mfupi (SMS) kwa huduma ya mawasiliano ya simu

### 1.3.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti

#### 1.3.1.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi

Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 na Disemba 2024 imeoneshwa hapo chini.

Kufikia Septemba 2024

Kufikia Disemba 2024

**Bilioni 41.1**

**Bilioni 42.5**

**3.3%** 

Kielelezo hapo juu kinaonesha kuongezeka kwa idadi ya dakika za huduma za sauti ndani ya nchi kwa 3.3% katika robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024.

#### Kielelezo 1.3.1.1 Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi

	Robo mwaka iliyoishia Septemba 2024	Robo mwaka iliyoishia Disemba 2024	Mabadiliko
Ndani ya mtandao	<b>Bilioni 21.1</b>	<b>Bilioni 21.0</b>	<b>-0.5%</b> ▼
Nje ya mtandao	<b>Bilioni 20.0</b>	<b>Bilioni 21.5</b>	<b>7.3%</b> ▲

Jedwali 1.3.1.1 linaonesha kuwa Disemba 2024 ulikuwa mwezi wenye idadi ya dakika nyingi zaidi ikilinganishwa na miezi mingine ya robo mwaka huo.


**Jedwali 1.3.1.1a Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani na nje ya mtandao nchini**

	Oktoba	Novemba	Disemba	Jumla
Ndani ya mtandao	7,195,009,769	6,729,276,557	7,065,895,010	20,990,181,336
Nje ya mtandao	7,173,195,427	7,009,966,097	7,304,796,308	21,487,957,832
<b>Jumla</b>	<b>14,368,205,196</b>	<b>13,739,242,654</b>	<b>14,370,691,318</b>	<b>42,478,139,168</b>


Jedwali 1.3.1 linaonesha takriban dakika bilioni 42.5 zilitumika katika robo mwaka iliyoishia Disemba 2024 ikilinganishwa na dakika bilioni 41.1 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2024. Katika kipindi hicho, idadi ya dakika nje ya mtandao ilikuwa kubwa zaidi ikilinganishwa na ndani ya mtandao katika robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024. Pia, Mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka na miaka mitano linaoneshwa kwenye jedwali 1.3.1.1b na 1.3.1.1c

Mgawanyo wa dakika ndani na nje ya mtandao nchini kwa kila mtoa huduma umeoneshwa kwenye Chati 1.3.1.1b na 1.3.1.1c. Airtel imeongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya dakika za ndani ya mtandao (38.2%) na nje ya mtandao (29.0%).

**Chati 1.3.1.1b Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti ndani ya mtandao kwa kila mtoa huduma**



**Chati 1.3.1.1c Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti nje ya mtandao kwa kila mtoa huduma**



**Jedwali 1.3.1.1b Mwenendo wa idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka**


	Machi - 24	Juni - 24	Septemba - 24	Disemba - 24
Ndani ya mtandao	18,493,328,620	21,344,770,781	21,088,541,912	20,990,181,336
Nje ya mtandao	16,470,309,864	18,224,300,276	20,033,335,066	21,487,957,832
<b>Jumla</b>	<b>34,963,638,484</b>	<b>39,569,071,057</b>	<b>41,121,876,978</b>	<b>42,478,139,168</b>

**Jedwali 1.3.1.1c Idadi ya dakika za huduma ya sauti ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita**

	2020	2021	2022	2023	2024
Ndani ya mtandao	54,561,254,851	51,673,651,476	62,678,814,642	77,770,241,513	81,916,822,649
Nje ya mtandao	27,084,539,242	43,194,917,029	60,064,367,493	67,100,445,506	76,215,903,038
<b>Jumla</b>	<b>81,645,794,093</b>	<b>94,868,568,505</b>	<b>122,743,182,135</b>	<b>144,870,687,019</b>	<b>158,132,725,687</b>

### 1.3.1.2 Idadi ya dakika za huduma ya sauti nje ya nchi

Idadi ya dakika kwenda na kutoka nje ya nchi imeoneshwa hapo chini.



Kielelezo kinaonesha kuongezeka kwa idadi ya dakika kwenda na kutoka nje ya nchi katika robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024. Idadi ya dakika kwenda nje ya nchi imeongezeka kwa 25%. Kwa upande mwingine, dakika kutoka nje ya nchi imeongezeka kwa 14%. Vilevile, takwimu zinaonesha kulikuwa na idadi kubwa ya dakika kwenda nje ya nchi ikilinganishwa na zilizotoka nje ya nchi.


Jumla ya dakika kwenda na kutoka Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW) kwa robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024 imeoneshwa katika Jedwali 1.3.1.2a. Pia, mwenendo wa idadi ya dakika ya huduma ya sauti kutoka na kwenda RoW inaoneshwa katika jedwali 1.3.1.2 b na 1.3.1.2c.

**Jedwali 1.3.1.2a Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW kwa robo mwaka inayoishia Disemba 2024**


	Oktoba	Novemba	Disemba	Jumla
Kwenda EA	40,897,298	39,373,516	44,212,977	<b>124,483,791</b>
Kutoka EA	10,454,047	10,374,892	9,859,129	<b>30,688,068</b>
Kwenda RoW	2,016,388	1,867,122	1,392,882	<b>5,276,392</b>
Kutoka RoW	2,157,484	2,220,872	2,264,476	<b>6,642,832</b>

Mgawanyo wa dakika kwenda na kutoka Afrika Mashariki (EA) na Mataifa Mengine (RoW) umeoneshwa kwenye Chati 1.3.2.2a na Chati 1.3.2.2b

**Chati 1.3.2.2a Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA**



**Chati 1.3.2.2b Mgawanyo wa dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka RoW**



### Jedwali 1.3.1.2b Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW kwa robo mwaka

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
Kwenda EA	65,842,203	71,779,120	101,188,767	124,483,791
Kutoka EA	24,421,366	26,759,182	26,794,839	30,688,068
Kwenda RoW	10,211,867	9,905,171	10,900,864	5,276,392
Kutoka RoW	6,034,528	6,148,575	6,032,139	6,642,832

### Jedwali 1.3.1.2c Idadi ya dakika za huduma ya sauti kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita

	2020	2021	2022	2023	2024
Kwenda EA	9,738,521	9,097,165	8,927,113	95,473,684	363,293,881
Kutoka EA	15,406,649	15,853,362	13,594,473	34,994,641	108,663,455
Kwenda RoW	38,014,133	24,856,947	26,034,131	19,510,999	36,294,294
Kutoka RoW	45,172,263	49,885,142	33,374,619	23,681,940	24,858,074

## 1.3.2 Idadi ya ujumbe mfupi wa maneno (SMS)

### 1.3.2.1 Idadi ya SMS ndani ya nchi

Robo mwaka inayoishia Septemba  
2024

**Bilioni 47.6**

Robo mwaka inayoishia Disemba  
2024

**Bilioni 52.9**

**11%** 

Robo mwaka	SMS ndani ya mtandao	SMS nje ya mtandao	Jumla
Julai - Septemba 2024	Bilioni 20.2	Bilioni 27.4	Bilioni 47.6
Oktoba - Disemba 2024	Bilioni 22.2	Bilioni 30.6	Bilioni 52.9
<b>Badiliko</b>	<b>10%</b>	<b>12%</b>	<b>11%</b>

Kielelezo kinaonesha kiujumla, idadi ya SMS imeongezeka kwa 11% kwa robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024

Jedwali 1.3.2.1a linaonesha mabadiliko ya idadi ya SMS ndani na nje ya mtandao. Mwezi Disemba 2024 ulikuwa na idadi kubwa ya SMS ikilinganishwa na miezi mingine kwenye kipindi husika.

### Jedwali 1.3.2.1a Idadi ya SMS ndani ya nchi

	Oktoba	Novemba	Disemba	Jumla
Ndani ya mtandao	7,115,791,516	7,147,296,226	7,983,200,491	<b>22,246,288,233</b>
Nje ya mtandao	9,715,029,143	9,728,014,930	11,201,131,635	<b>30,644,175,708</b>
<b>Jumla</b>	<b>16,830,820,659</b>	<b>16,875,311,156</b>	<b>19,184,332,126</b>	<b>52,890,463,941</b>

Mwenendo wa idadi ya SMS ndani ya nchi imeoneshwa katika jedwali 1.3.2.1b na 1.3.2.1c

### Jedwali 1.3.2.1b Mwenendo wa idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa kipindi cha robo mwaka

	Machi - 24	Juni - 24	Septemba - 24	Disemba - 24
Ndani ya mtandao	20,852,771,701	21,587,689,900	20,222,806,831	22,246,288,233
Nje ya mtandao	29,556,948,884	29,252,487,925	27,374,852,630	30,644,175,708
<b>Jumla</b>	<b>50,409,720,585</b>	<b>50,840,177,825</b>	<b>47,567,659,461</b>	<b>52,890,463,941</b>

### Jedwali 1.3.2.1c Idadi ya SMS za ndani ya nchi kwa miaka mitano iliyopita

	2020	2021	2022	2023	2024
Ndani ya mtandao	61,971,569,487	58,875,779,663	65,358,270,089	84,818,793,761	84,909,556,665
Nje ya mtandao	71,072,186,913	78,200,512,436	88,154,239,625	121,727,776,013	116,828,465,147
<b>Jumla</b>	<b>133,043,756,400</b>	<b>137,076,292,099</b>	<b>153,512,509,714</b>	<b>206,546,569,774</b>	<b>201,738,021,812</b>

### 1.3.2.2 Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA na RoW


Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA na RoW imeoneshwa kwenye Jedwali 1.3.2.2a. Pia, mwenendo wa SMS wa idadi wa SMS kutoka na kwenda EA na RoW umeoneshwa kwenye jedwali 1.3.2.2b na 1.3.2.2c.

### Jedwali 1.3.2.2a Idadi ya SMS kutoka na kwenda EA na RoW


	Oktoba	Novemba	Disemba	Jumla
Kwenda EA	154,042	155,066	185,343	<b>494,451</b>
Kutoka EA	2,450,535	2,653,484	3,043,500	<b>8,147,519</b>
Kwenda RoW	509,900	480,223	541,788	<b>1,531,911</b>
Kutoka RoW	525,227,010	517,834,529	505,569,662	<b>1,548,631,201</b>

Jedwali 1.3.3.2a linaonesha kuwa idadi kubwa ya SMS zilipokelewa kutoka EA na RoW kuliko zilizotumwa EA na RoW. Uwiano wa SMS zilizotumwa na kupokelewa umeoneshwa kwenye Chati 1.3.2.2a na 1.3.2.2b.

**Chati 1.3.2.2a Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka EA**



**Chati 1.3.2.2b Mgawanyo wa SMS kwenda na kutoka RoW**



**Jedwali 1.3.2.2b Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA na RoW kwa robo mwaka**

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
Kwenda EA	451,974	472,649	477,221	494,451
Kutoka EA	9,027,500	24,041,840	8,083,034	8,147,519
Kwenda RoW	1,390,335	1,651,119	1,131,776	1,531,911
Kutoka RoW	1,528,370,648	1,356,131,716	1,365,055,223	1,548,631,201

**Jedwali 1.3.2.2c Idadi ya SMS kwenda na kutoka EA na RoW kwa miaka mitano iliyopita**

	2020	2021	2022	2023	2024
Kwenda EA	1,235,692	1,425,624	1,700,525	2,233,288	1,896,295
Kutoka EA	50,880,982	89,717,530	58,344,672	37,592,410	41,662,728
Kwenda RoW	2,718,443	3,191,041	3,574,956	5,448,764	13,342,306
Kutoka RoW	3,935,379,714	4,599,468,894	4,664,200,079	5,562,047,440	5,798,188,788

**1.4 Kuzuru**

Sehemu hii inaonesha idadi ya dakika ya huduma ya sauti, SMS na Data kwa huduma za kuzuru (roaming).

**Kielelezo 1.4 Kuzuru**

	Dakika	SMS	Data
Kuzuru kwenda	<b>Bilioni 6.69</b>	<b>Milioni 10.93</b>	<b>5,557.87 PB</b>
Kuzuru Kutoka	<b>Bilioni 0.69</b>	<b>Milioni 8.35</b>	<b>188,168.48 PB</b>

**1.4.1 Kuzuru huduma ya sauti (dakika)**

Idadi ya dakika kwa huduma ya kuzuru ya sauti kwa robo mwaka iliyoishia Disemba 2024 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.1.

**Jedwali 1.4.1 Kuzuru huduma ya sauti (dakika)**

	EAC	SADC	RoW	Jumla
Kuzuru kwenda	13,298,382	18,846.12	6,675,581,904	<b>6,688,899,132</b>
Kuzuru Kutoka	564,252,725	4,999,385	121,897,049	<b>691,149,159</b>

**1.4.2 Kuzuru huduma ya SMS**

Idadi ya SMS kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Disemba 2024 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.2.

**Jedwali 1.4.2 Kuzuru huduma ya SMS**

	EAC	SADC	RoW	Jumla
Kuzuru kwenda	4,276,100	320,302	6,331,448	<b>10,927,850</b>
Kuzuru Kutoka	5,982,645	186,717	2,181,039	<b>8,350,401</b>

### 1.4.3 Kuzuru huduma ya intaneti

Idadi ya SMS kwa huduma za kuzuru kwa robo mwaka iliyoishia Disemba 2024 imeoneshwa kwenye jedwali 1.4.3.

#### Jedwali 1.4.3 Kuzuru huduma ya intaneti (megabytes)

	EAC	SADC	RoW	Jumla
Kuzuru kwenda	1,714,993	810,630.04	5,557,868,338,251	5,557,870,863,874
Kuzuru Kutoka	3,905,064,321,357	3,560,843,811,807	180,702,575,655,821	188,168,483,788,985

### 1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu

Vifaa vya masiliano vinavyotumia laini ya simu ndiyo kichocheo kikubwa katika kukuza matumizi ya huduma za mawasiliano ya simu/TEHAMA nchini. Idadi ya vifaa vilivyunganishwa kwenye mitandao ya simu imeoneshwa kwenye Jedwali 1.5.



#### Jedwali 1.5 Vifaa vya mawasiliano vinavyotumia laini za simu na kuunganishwa kwenye mtandao


Aina ya kifaa	Idadi ya Vifaa	Ueneaji (Penetration)
Simu za rununu (Feature phones)	56,862,957	87.39%
Simu janja (Smartphones)	23,419,299	35.99%
Handheld	1,628,133	2.50%
Modem	661,904	1.02%
Portable (including Personal Digital Assistant PDA)	56,229	0.09%
Tablet	480,097	0.74%
Module	53,184	0.08%
WLAN Router	206,049	0.32%
Dongle	97,457	0.15%
Internet of Things (IoT) Devices	147,102	0.23%
Vehicle	11,045	0.02%
Computer	12,473	0.02%
Wearable	8,474	0.01%
Device for the Automatic Processing of Data (APD)	3,734	0.01%

Kufikia Disemba 2024, asilimia ya simu janja (smartphones) kwa idadi ya watu imeongezeka hadi 35.99% kutoka 33.85% mwezi Septemba 2024. Aidha, asilimia ya simu za rununu (feature phones) imeongezeka kutoka 84.83% na kufikia 87.39%. Ueneaji wa vifaa vingine vya mawasiliano miongoni mwa watu ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.5.

### 1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu

Hadi kufikia Disemba 2024, idadi ya minara ya huduma ya mawasiliano ya simu ilikuwa ni 8,899. Mkoa wa Dar es Salaam uliongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya minara (1,214) kama inavyooneshwa kwenye ramani 1.6.

#### Ramani 1.6 Mgawanyo wa minara ya mawasiliano ya simu




## 1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu

Jedwali 1.7 linaonesha idadi ya mitambo ya 2G, 3G, 4G na 5G kwa kila mkoa hadi kufikia Disemba 2024 .

### Jedwali 1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi ya simu kimkoa

Mkoa	Idadi ya mitambo ya kurushia mawimbi			
	BTS (2G)	NodeB (3G)	eNB (4G)	gNB (5G)
<b>Tanzania Bara</b>				
Arusha	676	642	638	32
Dar-es-salaam	2,272	2,365	2,349	616
Dodoma	653	564	574	44
Geita	381	363	344	6
Iringa	379	335	338	4
Kagera	491	456	421	1
Katavi	157	135	140	1
Kigoma	471	423	400	3
Kilimanjaro	536	514	505	8
Lindi	338	257	280	1
Manyara	325	270	272	1
Mara	400	363	355	4
Mbeya	558	548	542	16
Morogoro	656	601	597	9
Mtwara	407	342	347	1
Mwanza	729	706	695	36
Njombe	299	265	263	3
Pwani	459	427	427	12
Rukwa	278	244	232	1
Ruvuma	427	348	352	2
Shinyanga	359	343	321	6
Simiyu	271	235	226	2
Singida	326	296	292	3
Songwe	234	203	199	13
Tabora	519	461	412	4
Tanga	613	536	538	3
<b>Zanzibar</b>				
Kaskazini Pemba	59	58	54	1
Kaskazini Unguja	78	80	77	4
Kusini Pemba	59	60	57	1
Kusini Unguja	113	113	111	4
Mjini Magharibi	184	209	204	58
<b>Jumla</b>	<b>13,707</b>	<b>12,762</b>	<b>12,562</b>	<b>900</b>

### Kielelezo 1.7 Mgawanyo wa mitambo ya kurushia mawimbi kwa teknolojia





Jedwali 1.7 linaonesha kuenea kwa kiasi kikubwa kwa teknolojia ya 2G na 3G, ikiwa na BTS 13,707 na NodeB 12,762. Japokuwa teknolojia ya 4G haijaenea kama 2G na 3G, idadi ya eNB za 4G zimefika 12,562. Aidha, gNB za 5G zimeongezeka kwa kiasi cha asilimia 7.9 zikiwa zimefika 900 na zimeenea zaidi katika maeneo ya mijini kama vile Dar es Salaam na Mjini Magharibi. Hata hivyo, Dar es Salaam inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya mitambo ya kurushia mawimbi ya mawasiliano kwa teknolojia zote (2G, 3G, 4G na 5G), na kuifanya kuwa kitovu cha mawasiliano nchini.

### 1.8 Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano

Uwekezaji katika miundombinu ya mawasiliano umeongeza usambaaji wa huduma ya Intaneti kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.8.

Jedwali 1.8 Ueneaji wa miundombinu ya mawasiliano kufikia Disemba 2024

		Septemba 2024	Disemba 2024
 <b>Asilimia ya watu waliofikiwa na huduma ya</b>	<b>2G</b>	<b>98.1%</b>	<b>98.2%</b>
	<b>3G</b>	<b>90.1%</b>	<b>91%</b>
	<b>4G</b>	<b>84.9%</b>	<b>88%</b>
	<b>5G</b>	<b>18%</b>	<b>20%</b>
 <b>Asilimia ya eneo lilofikiwa na huduma ya mawasiliano</b>	<b>2G</b>	<b>75%</b>	<b>75.1%</b>
	<b>3G</b>	<b>73.6%</b>	<b>73.8%</b>
	<b>4G</b>	<b>70.2%</b>	<b>71%</b>
	<b>5G</b>	<b>2.2%</b>	<b>2.5%</b>

Jedwali 1.8, linaonesha kuenea kwa wigo wa mawasiliano 2G, 3G, 4G na 5G kufikia 98.2%, 91%, 88%, na 20% ya watu nchini, mtawalia. Aidha, asilimia ya eneo lilofikiwa na mawasiliano ya 2G, 3G, 4G na 5G ni 75.1%, 73.8%, 71%, na 2.5%, mtawalia.

## 1.9 Huduma za Intaneti

### 1.9.1 Utumiaji wa Intaneti

Huduma ya intaneti inatolewa kwa kutumia laini za simu, waya (faiba), na mawimbi (wireless). idadi ya utumiaji wa intaneti inatokana na laini/waya ambazo zimetumia huduma ya Intaneti angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita, bila kujali teknolojia iliyotumika (FTTX, 2G - GPRS na EDGE, 3G, 4G, au 5G).

Idadi ya utumiaji wa Intaneti imeongezeka kwa 16% kutoka milioni 41.4 kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 hadi milioni 48 kwa robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024.

Kufikia Septemba 2024

Kufikia Disemba 2024

**Milioni 41.4**

**Milioni 48.0**

**16.1%** 

Idadi ya utumiaji wa Intaneti kwa robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.9.1a


#### Jedwali 1.9.1a Idadi ya utumiaji wa Intaneti kufikia mwisho wa kila mwezi katika robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024

Mwezi	Mobile Wireless	Fixed Wireless	Fixed Wired	Jumla
Oktoba	45,939,679	78,475	66,210	46,084,364
Novemba	46,784,789	80,780	75,187	46,940,756
Disemba	47,859,272	83,201	85,754	48,028,227


Kielelezo 1.9.1b linaonesha kuwa Intaneti ya kasi kwa huduma ya simu ndiyo njia inayopendelewa zaidi kupata Intaneti, ikiwa na laini 25,598,698 . Teknolojia ya 2G bado ina matumizi makubwa, ikiwa na laini 22,250,574. Teknolojia za Faiba Nyumbani (Fiber to the Home - FTTH) na Faiba Ofisini (Fiber to the Office - FTTO) zina idadi ndogo ya laini 71,661 na 11,540 mtawalia.

**Kielelezo 1.9.1a Matumizi ya Intaneti kwa teknolojia**


**Teknolojia ya kuhamishika**





**Teknolojia isiyohamishika**



**Chati 1.9.1a Mgawanyo wa huduma ya Intaneti kwa njia ya simu kwa kila mtoa huduma kwa robo mwaka inayoishia Disemba 2024**




### Chati 1.9.1b idadi ya laini za Intaneti (fixed) kwa kila mtoa huduma


Usajili wa intaneti ya waya unajumuisha usajili wa mtu binafsi na wa taasisi.

**Kielelezo 1.9.1b Idadi ya utumiaji wa huduma ya Intaneti kwa robo mwaka**




Kielelezo 1.9.1b inaonesha wastani wa ongezeko la 16.1% ya idadi ya utumiaji wa huduma ya intaneti kwa kila robo mwaka, ambapo utumiaji uliongezeka kutoka milioni 41.4 Septemba 2024 hadi milioni 48.0 Disemba 2024.

**Chati 1.9.1c Idadi ya laini zinazotumia huduma ya Intaneti kwa miaka mitano iliyopita**



**1.9.2 Matumizi ya huduma ya Intaneti**

Matumizi ya huduma ya Intaneti huhesabiwa kama kiasi cha data (katika Petabytes) kilichotumiwa katika kipindi husika. (1 Petabyte = 1000<sup>3</sup> Megabytes).



**Jedwali 1.9.2 Kiasi cha data kilichotumika katika robo ya mwaka inayoishia Disemba 2024**

	Oktoba	Novemba	Disemba
Kiasi cha data (GB)	200,518,094	200,567,905	215,501,720
usajili wa intaneti	46,084,364	46,940,756	48,028,227
GB kwa kila usajili	4.35	4.27	4.49

Jedwali 1.9.2 linaonesha kuwa kila usajili wa intaneti ulitumia wastani wa GB 4.49 kwa mwezi Disemba ambayo ni zaidi ikilinganiswaha na Oktoba na Novemba.

### 1.9.3 Uwezo wa kiunganishi cha Intaneti kimataifa


Uwezo wa kuunganisha huduma ya Intaneti kwenda nje na kuja ndani ya nchi (International Internet link capacity) unakuza matumizi ya Intaneti ndani na nje ya nchi. Jedwali 1.9.3 linaonesha kuwa nchi ina uwezo wa 15,331.68 Gbps kwa ajili ya uunganishaji wa huduma ya Intaneti. Hii inamaanisha ni asilimia 10.9 pekee ya uwezo wa viunganisho vya kimataifa ambao umetumika.

#### Jedwali 1.9.3 Uwezo wa kiunganishi cha huduma ya Intaneti

	Uwezo unaotoka (Gbps)	Uwezo unaoingia (Gbps)
Jumla ya uwezo uliopo	17,200.00	17,200.00
Jumla ya uwezo uliotumika	1,868.32	1,868.32
Uwezo unaopatikana kwa uunganishaji mpya	15,331.68	15,331.68

### 1.9.4 Kiashiria cha ubora wa huduma ya Intaneti

Wastani wa kasi ya kupakua na kupakia (katika Mbit/s) kama inavyooneshwa kwenye chati 1.9.4



### 1.9.5 Idadi ya viko vya Intaneti

Jumla ya idadi ya viko vilivyosajiliwa iliongezeka kutoka 31,584 mwishoni mwa Septemba 2024 hadi 32,267 mwishoni mwa Disemba 2024, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 1.9.5.

#### Jedwali 1.9.5 Idadi ya viko vya Intaneti

Kikoa	Septemba 2024	Disemba 2024
co.tz	24,796	25,195
or.tz	2,696	2,725
ac.tz	1,160	1,147
go.tz	913	918
.tz	1,706	1,950
sc.tz	256	273
ne.tz	33	33
me.tz	9	11
info.tz	2	2
hotel.tz	2	3
mobi.tz	5	4
tv.tz	2	2
mil.tz	4	4
<b>Jumla</b>	<b>31,584</b>	<b>32,267</b>


## 1.10 Huduma za Pesa Mtandao

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za pesa mtandao zinazotolewa na watoa huduma za pesa mitandao (Mobile Money Operators) kulingana na idadi ya akaunti za pesa mtandao na miamala.

### 1.10.1 Akaunti za pesa mtandao

Idadi ya akaunti za pesa mtandao ambazo zilitumika angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita iliongezeka kutoka akaunti milioni 60.8 katika robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 hadi milioni 63.2 katika robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024.

#### Kielelezo 1.10.1 Akaunti za pesa mtandao




#### Jedwali 1.10.1 Idadi ya akaunti za pesa mtandao

	Oktoba	Novemba	Disemba
Airtel Money	11,582,535	11,802,772	11,984,223
Azam Pesa	77,248	45,184	32,418
HaloPesa	5,317,112	5,553,962	5,696,951
Mixx by Yas	19,177,882	19,367,125	19,384,781
T- Pesa	1,464,589	1,482,764	1,508,952
M-pesa	22,548,857	23,402,837	24,600,244
<b>Jumla</b>	<b>60,168,223</b>	<b>61,654,644</b>	<b>63,207,569</b>

Jedwali 1.10.1 linaonesha kuwa akaunti za pesa mtandao ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 2.3 kwa mwezi katika robo mwaka iliyoishia Disemba 2024. Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao umeoneshwa kwenye Chati 1.10.1.

#### Chati 1.10.1 Mgawanyo wa akaunti za pesa mtandao



Chati 1.10.1 inaonesha kuwa soko la pesa mtandao lina ushindani, huku M-pesa ikiongoza kwa kuwa na asilimia 39.8.

### 1.10.2 Idadi ya miamala ya pesa mtandao

Idadi ya miamala ya pesa mtandao kwa akaunti zilizoweka na kutuma pesa kwa njia ya pesa mtandao katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ya robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024 imeoneshwa kwenye Jedwali 1.10.2a. Pia, mwenendo wa idadi ya miamala na akaunti kwa robo mwaka na miaka mitano imeoneshwa kwenye jedwali 1.10.2b na 1.10.2c.

#### Jedwali 1.10.2a Idadi ya miamala ya pesa mtandao

	Oktoba	Novemba	Disemba
Airtel Money	101,773,680	99,438,660	104,187,370
Azam Pesa	1,657,911	1,335,356	1,638,250
HaloPesa	36,389,613	36,581,657	39,059,824
T- Pesa	518,742	511,508	633,850
M-pesa	131,407,742	130,749,560	136,898,193
Mixx by Yas	96,397,449	85,123,969	96,396,871
<b>Jumla</b>	<b>368,145,137</b>	<b>353,740,710</b>	<b>378,814,358</b>

#### Jedwali 1.10.2b Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa robo mwaka

Robo mwaka	Idadi ya akaunti	idadi ya miamala
Machi 2024	52,990,091	1,370,558,108
Juni 2024	55,732,728	873,033,652
Septemba 2024	60,815,533	879,361,166
Disemba 2024	63,207,569	1,100,700,205

#### Jedwali 1.10.2c Idadi ya usajili na miamala ya pesa mtandao kwa miaka mitano iliyopita

Mwaka	Idadi ya akaunti	Idadi ya miamala
2020	32,268,630	3,412,210,062
2021	35,285,767	3,752,084,894
2022	40,953,496	4,195,899,414
2023	52,875,129	5,273,086,154
2024	63,207,569	3,737,202,434

## 1.11 Ubora wa huduma za simu na Intaneti


Vipimo vya ubora wa huduma (Quality of Service - QoS) ya simu na Intaneti zinazotolewa na mitandao ya simu nchini vilifanyika kuanzia Oktoba hadi Disemba 2024 kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa huduma (QoS) na mbinu za vipimo zilizoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2018.

### 1.11.1 Upatikanaji wa mtandao

Upatikanaji wa mtandao ni kiashiria kinachoonesha upatikanaji wa mtandao wa simu wakati watumiaji wanataka kutumia huduma za mtandao huo. Lengo ni kufikia zaidi ya 99%.

Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane kati ya maeneo maeneo yaliyopimwa. Airtel na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na saba. Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya kumi na tisa, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.1.

Chati 1.11.1. Upatikanaji wa Mtandao (%) (Lengo ni zaidi ya 99%)




### 1.11.2 Simu zilizoshindwa kuunganishwa

Simu zilizoshindwa kuunganishwa hupimwa kwa asilimia ya simu ambazo hazikuweza kuunganishwa baada ya kupiga kwa sababu za kiufundi. Lengo ni chini ya 2%.

Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika. Halotel and Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane, Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na saba, na TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo matano kati ya maeneo kumi na nane yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.2.

**Chati 1.11.2 Simu zilizoshindwa kuunganishwa**




**1.11.3 Simu zilizokatika**

Simu zilizokatika hupimwa kwa asilimia ya simu zinazokatika kwa sababu za kiufundi kabla ya wahusika kumaliza mazungumzo yao. Lengo ni chini ya 2%.

Airtel, Yas, Vodacom na Halotel walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika, TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.3.

**Chati 1.11.3. Matokeo ya Simu zilizokatika**




**1.11.4 Upatikanaji wa huduma ya 2G**

Upatikanaji wa huduma ya 2G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 2G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 2G ni -85 dBm.

Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya kumi na nane ambapo vipimo vilifanyika. Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tatu kati ya maeneo kumi na nne, Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo nane kati ya maeneo tisa, TTCL ilifikia lengo kwenye eneo moja kati ya manne yaliyopimwa kama inavyooneshwa Chati 1.11.4.

**Chati 1.11.4. Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma**




### 1.11.5 Upatikanaji wa huduma ya 3G

Upatikanaji wa huduma ya 3G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Wateja hawawezi kupata huduma za mtandao wa simu za 3G katika maeneo ambayo hayana mtandao au yenye mtandao duni. Lengo la juu kwa teknolojia ya 3G ni -85 dBm.

Halotel na Yas zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambayo vipimo vilifanyika. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane, Airtel na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na saba kati ya maeneo kumi na tisa, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.5.

**Chati 1.11.5. Matokeo ya kulinganisha upatikanaji wa huduma ya**




### 1.11.6 Upatikanaji wa huduma ya 4G

Upatikanaji wa huduma ya 4G huonesha jinsi maeneo yaliyofikiwa na huduma hiyo na watoa huduma wa mtandao wa simu. Lengo la juu kwa teknolojia ya 4G ni -95 dBm.

Yas na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane kati ya kumi na tisa. Halotel na Airtel zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na saba kati ya maeneo kumi na tisa yaliyopimwa kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.6.

Chart 1.11.6. Matokeo linganishi kwenye upatikanaji wa huduma ya 4G




### 1.11.7 Simu zilizofanikiwa

Simu zilizofanikiwa hupimwa kwa asilimia ya simu zilizokamilishwa baada ya upigaji, kwamba hazikuzuiwa au kukatika. Lengo ni sawa na au zaidi ya 95%.

Airtel, Yas na Halotel zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa yaliyopimwa. Vodacom ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane, TTCL ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na tatu kati ya kumi na nane, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.7.

Chati 1.11.7. Matokeo ya kulinganisha simu zilizofanikiwa




### 1.11.8 Simu kuhamishika

Simu kuhamishika hupimwa kwa jinsi simu za sauti zinavyohamishwa kutoka mnara mmoja wa mawasiliano hadi mwingine bila kukatika pale mtumiaji anapotoka eneo moja kwenda jingine. Lengo ni sawa na au zaidi ya 98%.

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.8.

Chati 1.11.8. Matokeo ya kulinganisha simu kuhamishika




### 1.11.9 Ubora wa Sauti

Ubora wa Sauti ni kipimo cha utambuzi wa ubora wa sauti wakati wa mazungumzo ya simu. Kiwango cha alama ya ubora wa sauti ni kati ya 1 hadi 5, huku 1 ikiwa duni na 5 ikiwa ni ubora mzuri wa sauti. Lengo ni wastani wa sampuli zote za vipimo vya ubora wa sauti kuwa zaidi ya 3.5.

Airtel, Yas, na Vodacom zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na moja ambapo vilipimo vilifanyika, Halotel na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi ambayo vipimo vilifanyika kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.9.

Chati 1.11.9. Matokeo ya kulinganisha kwenye Ubora wa Sauti




### 1.11.10 Kasi ya kupakua data

Kasi ya kupakua data ni kipimo cha kasi ya uhamishaji data kwenye mtandao. Hupima jinsi data inavyohamishwa haraka kutoka kwa itifaki (protocol) ya uhamishaji faili (File Transfer Protocol - FTP) hadi kwa kifaa cha mawasiliano ya simu. Lengo ni wastani kuwa sawa au zaidi ya 4000 Kbps.

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.10.

Chati 1.11.10. Matokeo linganishi kwenye kasi ya kupakua data




### 1.11.11 Muda wa kupata huduma ya data

Muda wa kupata huduma ya data hupimwa kwa muda ambao kifaa cha mtumiaji huchukua kutuma ombi na kupokea jibu kutoka kwenye seva. Lengo ni wastani kuwa chini ya 400ms.

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikisha lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.11.

Chati 1.11.11. Matokeo linganishi ya muda wa kupata huduma ya data




### 1.11.12 Simu kushindwa kusoma mtandao

Simu kushindwa kusoma mtandao hupimwa kwa asilimia ambayo simu ya mkononi inaposhindwa kuunganishwa kwenye mtandao ikiwa imewashwa. Lengo ni chini ya 2%.

Yas ilifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika. Airtel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane kati ya kumi na tisa. Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na saba kati ya maeneo kumi na tisa, Vodacom na TTCL zilifikia lengo kwenye maeneo kumi na sita kati ya kumi na tisa, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.12.

Chati 1.11.12. Matokeo ya kulinganisha simu kushindwa kusoma mtandao




### 1.11.13 Muda wa simu kusoma mtandao

Muda wa simu kusoma mtandao ni muda ambao simu ya mkononi inachukua kuunganishwa kwenye mtandao ikiwa imewashwa. Lengo ni chini ya sekunde 5 (<5s).

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambapo vipimo vilifanyika, wakati Halotel ilifikia lengo kwenye maeneo kumi na nane kati ya maeneo kumi na tisa, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.13.

Chart 1.11.13. Matokeo ya kulinganisha muda wa simu kusoma mtandao




### 1.11.14 Muda wa kuanzisha simu

Muda wa kuanzisha simu hupimwa kwa muda ambao simu inachukua kuunganishwa baada ya kupiga. Lengo ni chini ya sekunde 10.

Watoa huduma wote wa mawasiliano ya simu walifikia lengo kwenye maeneo yote kumi na tisa ambayo vipimo vilifanyika, kama inavyooneshwa kwenye Chati 1.11.14.

**Chart 1.11.14. Matokeo ya kulinganisha muda wa kuanzisha simu**



Matokeo ya upimaji wa ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2024 yanaonesha kuwa Yas ilikua na 100%, Vodacom 97%, Airtel na Halotel walikua 96%, na TTCL 89%, kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali 1.11.1.

#### Jedwali 1.11.1 Matokeo ya ubora wa huduma za simu na Intaneti kwa robo mwaka iliyoishia Disemba 2024

Mtoa huduma	Kiwango cha ufanisi
Yas	100%
Vodacom	97%
Halotel	96%
Airtel	96%
TTCL	89%
Wastani wa Sekta	96%

## 1.12 Majaribio ya ulaghai

### Tanzania Bara

Mkoa	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Jumla
Rukwa	2,200	404	465	1,667	569	5,305
Morogoro	1,833	13	733	14	1,685	4,278
Mbeya	451	63	55	214	147	930
Dar es Salaam	436	24	134	38	133	765
Katavi	0	41	4	198	38	281
Arusha	43	3	17	14	183	260
Songwe	0	87	33	30	0	150
Mwanza	51	3	20	10	48	132
Tabora	18	10	4	81	9	122
Kilimanjaro	13	5	26	7	39	90
Iringa	33	34	8	7	3	85
Pwani	14	2	26	12	8	62
Kagera	21	3	11	15	11	61
Dodoma	12	17	13	4	2	48
Kigoma	7	7	5	9	15	43
Tanga	12	6	19	2	2	41
Njombe	0	8	10	13	4	35
Shinyanga	17	6	2	5	1	31
Ruvuma	3	2	10	14	0	29
Mtwara	5	4	9	7	0	25
Singida	2	2	11	5	1	21
Geita	0	3	5	10	1	19
Lindi	2	1	6	7	1	17
Mara	4	2	6	3	2	17
Manyara	8	1	3	2	0	14
Simiyu	0	1	5	1	0	7
Morogoro	2	1	10	2	0	15

### Zanzibar

Mjini Magharibi	2	1	10	2	0	15
Kaskazini Unguja	0	0	5	0	0	5
Kusini Unguja	0	0	5	0	0	5
Kusini Pemba	0	0	2	0	0	2
Kaskazini Pemba	0	0	1	0	0	1
<b>Jumla</b>	<b>5,187</b>	<b>753</b>	<b>1,663</b>	<b>2,391</b>	<b>2,902</b>	<b>12,896</b>


Kielelezo hapo chini kinaonesha majaribio ya ulaghai kwa kila mtoa huduma kwa robo ya mwaka iliyoishia Septemba 2024 na Disemba 2024. Airtel ilikuwa na idadi ya majaribio mengi zaidi ya watoa huduma wengine.

Robo ya mwaka inayoishia	Airtel	Halotel	Yas	TTCL	Vodacom	Jumla
Disemba 2024	5,187	753	1,663	2,391	2,902	12,896
Septemba 2024	3,408	711	6,581	2,127	3,175	16,002
Badiliko	52%	6%	-75%	12%	-9%	-19%

Takwimu zinaonesha kuwa majaribio ya ulaghai kwa ujumla yamepungua kwa wastani wa 19%. Chati 1.12a inaonesha majaribio ya ulaghai kimkoa. Mikoa ya Rukwa na Morogoro ndiyo inayoongoza, ikiwa na zaidi ya theluthi moja ya majaribio yote ya ulaghai nchini. Pia, takwimu zinaonesha kuwa matukio ya ulaghai kwa Halotel, TTCL, Airtel yameongezeka kwa 6%, 12% and 52% mtawalia. Aidha, matukio ya ulaghai kwa Yas na Vodacom yamepungua kwa 75% na 9% mtawalia.

### Chati 1.12a Idadi majaribio ya ulaghai kimkoa kwa robo mwaka inayoishia Disemba 2024

#### Tanzania Bara



**Rukwa and Morogoro ziliongoza kwa kuwa na majaribio mengi ya ulaghai kifuatiwa na Mbeya, Dar es Salaam na Katavi.**

**Mikoa ya Kusini Unguja, Kusini Pemba na Kaskazini Pemba zilikuwa na idadi ndogo ya majaribio ya ulaghai.**

#### Zanzibar


Mjini Magharibi	15
Kaskazini Unguja	5
Kusini Unguja	5
Kusini Pemba	2
Kaskazini Pemba	1

**Jedwali 1.12b Majaribio ya ulaghai kiwilaya kwa mikoa minne inayoongoza**

Region	District	Fraudulent attempts
<b>Rukwa</b>	Kalambo	140
	Nkasi	287
	Sumbawanga vijijini	1,083
	Sumbawanga mjini	3,795
<b>Morogoro</b>	Gairo	3
	Kilombero	4,101
	Kilosa	37
	Morogoro vijijini	1
	Morogoro mjini	105
	Mvomero	4
	Ulanga	17
	Malinyi DC	7
	Mlimba DC	3
<b>Mbeya</b>	Chunya	63
	Kyela	22
	Mbarali	30
	Mbeya vijijini	251
	Mbeya mjini	536
	Rungwe	28
<b>Dar es Salaam</b>	Ilala	155
	Kigamboni	6
	Kinondoni	387
	Temeke	119
	Ubungo	98

### Chati 1.12b Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma

Mgawanyo wa asilimia ya majaribio ya ulaghai mtandaoni kwa kila mtoa huduma umeoneshwa katika Chati 1.12b.



### 1.13 Leseni za Mawasiliano ya simu na Intaneti

Mawasiliano ya simu na Intaneti		
Aina ya leseni	Idadi ya leseni	
	Septemba 2024	Disemba 2024
Network Facilities Licences	35	37
Network Services Licences	16	18
Application Services Licences	146	155
Aircraft Stations	176	178
Amateur Stations	23	17
Fixed VSAT Terminals	36	36
Mobile VSAT Terminals	2	2
Satellite Ground Earth Stations	1	1
Ship Stations	36	30
HF Radio Stations	21	19
VHF- UHF Radio Repeaters	2	2
VHF - UHF Radio Station with Pair of Frequency	109	107
VHF - UHF Radio Station with Single Frequency	184	190
Numbering	493	514

### 1.14 Vyeti

Aina ya cheti na idadi		
Aina ya cheti	Idadi ya vyeti	
	Septemba 2024	Disemba 2024
Global Maritime Distress and Safety Systems	177	196
Type Approval	4774	4,948
Registration for Satellite Mobile Phones	32	46

# Sura ya pili


## Huduma za Utangazaji



## 2. Huduma za Utangazaji

Sehemu hii inawasilisha takwimu za huduma za televisheni kwa njia ya mitambo iliyosimikwa ardhini (DTT), setilaiti (DTH), na kwa njia ya waya (Cable TV).

### Kielelezo 2.0 Mgawanyiko wa visimbuzi vilivyolipiwa



### 2.1 Visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu

Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu iliyopita ili kupata huduma za utangazaji za televisheni imeoneshwa kwenye Jedwali 2.1. Jedwali linaonesha kuwa Azam Media Limited ina idadi kubwa ya visimbuzi vya DTT vilivyolipiwa vifurushi ikilinganishwa na watoa huduma wengine, ikifuatiwa na Star Media Limited. Aidha, Azam Media Limited ina idadi kubwa ya visimbuzi vya DTH vilivyolipiwa ikilinganishwa na watoa huduma wengine, ikifuatiwa na Star Media Limited. Kwa ujumla idadi ya visimbuzi vya DTH vilivyolipiwa vifurushi ni vingi kuliko visimbuzi vya DTT.


### Jedwali 2.1 Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu

	Visimbuzi vya DTT	Visimbuzi vya DTH	Jumla ya visimbuzi vilivyolipiwa
Azam Media Limited	294,775	1,045,360	<b>1,340,135</b>
Basic Transmissions Limited (Continental)	36,413	31,250	<b>67,663</b>
Multichoice Tanzania Limited (DStv)	0	225,263	<b>225,263</b>
Star Media Limited	232,494	245,033	<b>477,527</b>
Zuku	0	21,335	<b>21,335</b>
<b>Jumla</b>	<b>563,682</b>	<b>1,568,241</b>	<b>2,131,923</b>

Agape Associates Limited na Basic Transmissions Limited (Digitek) hawakuwa na visimbuzi vilivyolipiwa angalau mara moja katika kipindi cha miezi mitatu

Ramani 2.1 inaonesha idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa. Dar es Salaam ina visimbuzi vingi (694,257), ikifuatiwa na Mwanza (173,187), Mbeya (147,660), Arusha (135,929) na mikoa mingine ni kama ilivyooneshwa kwenye ramani.


### Ramani 2.1 Idadi ya visimbuzi vilivyolipiwa vifurushi kwa kila mkoa



### 2.2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya

Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya (Cable TV subscriptions) zimepungua kwa 12% kutoka 19,153 kwa robo mwaka inayoishia Septemba 2024 na kufikia 16,767 katika kipindi cha robo mwaka inayoishia Disemba 2024.

**Kielelezo 2.2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya**




Kufikia Septemba 2024	Kufikia Disemba 2024
19,153	16,767



Idadi ya televisheni kwa kila mkoa katika kipindi husika imeoneshwa kwenye Chati 2.2.

**Chati 2.2 Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kufikia Disemba 2024**



Kwa mikoa yote Tanzania Bara, Shinyanga inaongoza kwa kuwa na televisheni nyingi zinazopokea maudhui kwa njia ya waya (4,219), ikifuatiwa na Mwanza (2,070) na Tabora (1,872).

Mwenendo wa idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya zimeoneshwa kwenye Jedwali 2.2a na 2.2b.

**Jedwali 2.2a Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa robo mwaka**

	Machi 2024	Juni 2024	Septemba 2024	Disemba 2024
Usajili	15,781	18,820	19,153	16,767

**Jedwali 2.2b Idadi ya televisheni zilizounganishwa kwa njia ya waya kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita**

	2020	2021	2022	2023	2024
Usajili	14,350	19,739	22,295	16,223	16,767

## 2.3 Ueneaji wa huduma za utangazaji

Takwimu zinaonesha kuna utofauti wa ueneaji wa huduma za utangazaji kwa njia ya DTT, DTH na redio kama inavyoonekana kwenye Jedwali 2.3.

### Jedwali 2.3 Ueneaji wa huduma za utangazaji hadi kufikia Disemba 2024

Kiashiria	Disemba 2024
% ya watu waliofikiwa na DTT	58%
% ya watu waliofikiwa na DTH	100%
% ya watu waliofikiwa na redio za FM	78.3%
% ya eneo lililofikiwa na DTT	33%
% ya eneo lililofikiwa na DTH	100%
% ya eneo lililofikiwa na redio za FM	56.7%

## 2.4 Utekelezaji wa masharti ya leseni ya utangazaji

Ufuatiliaji wa maudhui kwa watoa huduma za utangazaji wa kitaifa nchini ulifanyika kuanzia Oktoba hadi Disemba 2024 kwa kuzingatia vigezo vya QoS na mbinu za vipimo vilivyoainishwa kwenye Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Ubora wa Huduma), 2018.

### 2.4.1 Uwasilishaji na uzingatiaji wa ratiba ya vipindi

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuwasilisha ratiba ya vipindi ikionesha muda, mpangilio, na idadi, na kuzingatia ratiba ya vipindi wanavyokusudia kurusha hewani. Uzingatiaji wa uwasilishaji wa mpangilio wa vipindi na kufuata ratiba kwa robo mwaka iliyotathminiwa umeonyeshwa kwenye Jedwali 2.4.1a na 2.4.1b.

### Jedwali 2.4.1a Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya televisheni

TV	Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi	Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi
ITV	Haijakidhi	Haijakidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten	Haijakidhi	Haijakidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Haijakidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi
Arise and Shine	Imekidhi	Imekidhi
WRM TV	Haijakidhi	Haijakidhi
Clouds TV	Imekidhi	Haijakidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Haijakidhi
Upendo TV	Imekidhi	Haijakidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Haijakidhi
Channel Ten Plus	Haijakidhi	Haijakidhi
TVE	Imekidhi	Haijakidhi

**Jedwali 2.4.1b Uwasilishaji na uzingatiaji wa mpango wa vipindi vya redio**

Redio	Uwasilishaji wa ratiba ya vipindi	Uzingatiaji wa ratiba ya vipindi
Radio One	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Haijakidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi
EFM	Imekidhi	Haijakidhi
Wasafi FM	Haijakidhi	Haijakidhi
Magic FM	Imekidhi	Imekidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi
Radio Maria	Imekidhi	Imekidhi

**2.4.2 Utofauti wa vipindi, maudhui ya elimu na uzingatiaji wa dakika tisini ya utoaji wa habari**

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kutoa maudhui anuai ili kukidhi tamaduni na mahitaji ya rika tofauti. Pia wanatakiwa kutoa maudhui ya elimu na kutenga muda wa dakika tisini kwa ajili wa habari na matukio. Uzingatiaji wa uanuai wa vipindi kwa robo mwaka

**Jedwali 2.4.2a Uanuai wa vipindi vya televisheni**

TV	Utofauti wa vipindi	Maudhui ya elimu	Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari
ITV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Arise and Shine	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi
WRM TV	Haijakidhi	Haijakidhi	Imekidhi
Clouds TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Upendo TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Channel Ten Plus	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi
TVE	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

### Jedwali 2.4.2b Uanuai wa vipindi vya redio

Redio	Utofauti wa vipindi	Maudhui ya elimu	Uzingatiaji wa dakika tisini wa habari
Radio One	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Wasafi FM	Imekidhi	Imekidhi	Haijakidhi
Magic FM	Haijakidhi	Haijakidhi	Haijakidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Maria	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

### 2.4.3 Uzingatiaji wa maudhui ya ndani (local content)

Watoa huduma za utangazaji wenye leseni za kitaifa (national broadcasters) wanatakiwa kuhakikisha kwamba asilimia 60 ya vipindi vyao vimetengenezwa ndani ya nchi, ili kuchagiza utamaduni, lugha, na maudhui ya ndani ya nchi. Matokeo ya upimaji ya uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwa robo mwaka yameoneshwa kwenye Jedwali 2.4.3a na Jedwali 2.4.3b.

### Jedwali 2.4.3a Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya televisheni

TV	Yenye manufaa kwa jamii	Lugha (Kiswahili au Kiingereza)	60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani
ITV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
UTV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Tumaini TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Star TV Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC 1	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TV Imaan	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Arise and Shine	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
WRM TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Clouds TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Hope Channel Tanzania	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Upendo TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Mahaasin TV	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Channel Ten Plus	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TVE	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

**Jedwali 2.4.3b Uzingatiaji wa maudhui ya ndani kwenye vipindi vya redio**

Redio	Yenye manufaa kwa jamii	Lugha (Kiswahili au Kiingereza)	60% ya uzalishaji wa maudhui ya ndani
Radio One	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC Taifa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Adventist World Radio (AWR)	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Clouds FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
East Africa Radio	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
EFM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Wasafi FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Magic FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
TBC International	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Free Africa	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Bongo FM	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi
Radio Maria	Imekidhi	Imekidhi	Imekidhi

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

**2.5 Leseni za Utangazaji**

Aina ya leseni	Idadi ya leseni	
	Septemba 2024	Disemba 2024
National Content Television (FTA) Licences	16	17
District Content Television (FTA) Licences	22	21
National Content Radio Licences	14	14
Regional Content Radio Licences	33	33
District Content Radio Licences	182	186
Community Radios	17	17
Community Televisions	-	-
National Content Televisions by Subscription	28	28
District Content Televisions by Subscription	1	1
National Content (support services)	3	3
Online Content Aggregators	6	6
Weblogs (Blogs)	66	66
Online Radios	10	10
Online Televisions	210	199
Cable Televisions	63	58

# Sura ya tatu

**Huduma za Posta na Usafirishaji  
wa vifurushi na vipeto**



## 3. Huduma za Posta na Usafirishaji wa Vifurushi na Vipeto

VIWANGO VYA ISO 9001: 2015

Sehemu hii inawasilisha takwimu za masanduku ya posta, wateja, huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto, zilizotumwa na kupokelewa, kwenda na kutoka ndani ya nchi, Afrika Mashariki (EA) na mataifa mengine (RoW).

### 3.1 Idadi ya masanduku ya posta

Shirika la Posta Tanzania (TPC) linatoa huduma za msingi za posta za masanduku na mifuko binafsi ya barua kwa watu binafsi na kampuni. Idadi ya masanduku na mifuko binafsi katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba 2024, ni kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 3.1.

#### Jedwali 3.1 Masanduku na mifuko binafsi ya barua

Mwezi	Masanduku ya barua	Mifuko binafsi ya barua	Jumla
Oktoba	158,006	47	158,053
Novemba	158,006	47	158,053
Disemba	158,006	47	158,053

### 3.2 Wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto katika kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba imeoneshwa kwenye Jedwali 3.2.

#### Jedwali 3.2 Idadi ya wateja wa huduma ya usafirishaji wa vifurushi/vipeto

Mwezi	Kampuni/Taasisi	Wateja binafsi	Jumla
Oktoba	1,260	51,528	52,788
Novemba	1,160	53,341	54,501
Disemba	969	62,697	63,666

Jedwali 3.2 inaonesha kuwa wateja binafsi ni wengi zaidi kuliko wateja wa makampuni/taasisi

### 3.3 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa

#### 3.3.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi


Takwimu zinaonesha Barua (Letter) zilitumwa zaidi katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Disemba 2024, ikifuatiwa na Nyaraka (Document). Vipeto (Packets) vimetumwa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi hicho. Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa katika kipindi husika zimeoneshwa kwenye Jedwali 3.3.

### Jedwali 3.3.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi kwa robo mwaka iliyoishia Disemba 2024

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Oktoba	63,094	49,807	2,877	49,569	103	165,450
Novemba	49,095	32,893	3,650	44,265	2,042	131,945
Disemba	56,794	47,159	5,593	52,170	13,105	174,821
Jumla	168,983	129,859	12,120	146,004	15,250	472,216

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa na TPC na watoa huduma wengine wa huduma za usafirishaji ndani ya nchi umeoneshwa katika Chati 3.3. TPC ikiwa na idadi kubwa zaidi (63.6%) ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi ikilinganishwa na watoa huduma binafsi (36.4%).

### Chati 3.3 Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa ndani ya nchi



### 3.3.2 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kupitia TPC na watoa huduma wengine wa huduma ya usafirishaji katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2024 imeoneshwa kwenye jedwali 3.3.2a.

#### Jedwali 3.3.2a Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi kwa mtoa huduma

Watoa huduma	Jul - Sept 2024	Okt- Dis 2024
TPC	18,483	47,399
Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto	15,083	16,595
Jumla	33,566	63,994

Jedwali 3.4b linaonesha idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi. Takwimu zinaonesha kuwa barua zimetumwa zaidi nje ya nchi katika robo mwaka iliyoishia Disemba 2024, ikifuatiwa na nyaraka.

#### Jedwali 3.3.2b Idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Oktoba	9,303	578	93	1,213	214	11,401
Novemba	14,854	4,345	1,117	4,079	394	24,789
Disemba	19,841	3,912	198	3,783	70	27,804
Jumla	43,998	8,835	1,408	9,075	678	63,994

### 3.4 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa

#### 3.4.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka ndani ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kupitia TPC na watoa huduma wengine wa usafirishaji wa vifurushi na vipeto ilikuwa 480,757.

#### Jedwali 3.4.1 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa ndani ya nchi kwa robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Oktoba	48,039	48,216	2,685	51,611	7	150,558
Novemba	45,369	31,954	4,164	41,756	1,738	124,981
Disemba	77,735	45,305	5,413	63,873	12,892	205,218
<b>Jumla</b>	<b>171,143</b>	<b>125,475</b>	<b>12,262</b>	<b>157,240</b>	<b>14,637</b>	<b>480,757</b>

#### 3.4.2 Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi ni 93,527 kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Disemba 2024 kama ilivyooneshwa kwenye jedwali 3.4.2a.

#### Jedwali 3.4.2a Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa watoa huduma

Watoa huduma	Jul - Sept	Okt - Dis
TPC	38,668	53,390
Watoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto	22,044	40,137
<b>Jumla</b>	<b>60,712</b>	<b>93,527</b>


Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi zimeoneshwa kwenye Jedwali 3.4.2b. Barua kutoka nje ya nchi zimepokelewa kwa idadi kubwa zaidi ikilinganisha na bidhaa nyingine katika robo ya mwaka iliyoishia Disemba 2024, wakati mizigo kutoka nje ya nchi ilipokelewa kwa idadi ndogo zaidi katika kipindi husika.

#### Jedwali 3.4.2b Idadi ya bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi kwa aina ya huduma

Mwezi	Barua	Vifurushi	Vipeto	Nyaraka	Mizigo	Jumla
Oktoba	12,841	1,679	2,341	610	218	17,689
Novemba	42,794	5,869	4,395	805	190	54,053
Disemba	10,837	3,112	5,977	1,824	35	21,785
<b>Jumla</b>	<b>66,472</b>	<b>10,660</b>	<b>12,713</b>	<b>3,239</b>	<b>443</b>	<b>93,527</b>

Mgawanyo wa idadi ya bidhaa za kiposta zilizotumwa na kupokelewa unaonesha kuwa Tanzania ilituma bidhaa za kiposta chache zaidi nje ya nchi (40.6%) kuliko ilivyopokea (59.4%) kama ilivyooneshwa kwenye Chati 3.4

### Chati 3.4 Mgawanyo wa bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi na kupokelewa kutoka nje ya nchi



■ Bidhaa za kiposta zilizotumwa nje ya nchi  
 ■ Bidhaa za kiposta zilizopokelewa kutoka nje ya nchi

### 3.5 Ubora wa huduma za Posta na Usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Katika kipindi cha robo mwaka kilichoishia Disemba 2024, vipimo vya Ubora wa Huduma (QoS) vilifanyika katika kanda A na B ili kutathmini jinsi huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto zilivyokidhi viwango vya utoaji huduma vilivyowekwa kwenye kanuni za ubora.

Kanda A (Inter-Town Zone A) inayojumuisha miji ya Arusha, Moshi, Tanga, Morogoro, Kibaha, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Iringa, na Unguja, kiwango kinahitaji 85% ya bidhaa zipokelewe siku inayofuata (D+1). Kanda B (Inter-Town Zone B), inayojumuisha miji ya Tabora, Shinyanga, Kahama, Bariadi, Geita, Singida, Bukoba, Musoma, Kigoma, Mtwara, Lindi, Songea, Sumbawanga, Songwe, Mpanda, Babati, Njombe, Mkoani, na Chakechake, kiwango kinahitaji 88% ya bidhaa zipokelewe ndani ya siku tatu (D+3). Matokeo ya upimaji yameoneshwa kwenye jedwali 3.5a na 3.5b.

#### Jedwali 3.5a Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda A (85% ya bidhaa zipokelewe siku inayofata (D+1))

Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi	Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda A
Little Tanzania Limited	Imekidhi
Tanzmovers Limited	Imekidhi
Kimbinyiko International Co. Ltd	Imekidhi
Mwanga Logistics And Distribution Ltd	Imekidhi
Madeira Courier Services	Imekidhi
Blaze Concierge And Courier Services Limited	Imekidhi
Simba Logistic Equipment Supply Co. Ltd	Imekidhi
Segax Group Limited	Imekidhi
Sga Cash In Transit (T) Limited	Haijakidhi
Ellymo Company Limited	Haijakidhi
Kleafast couriers and logistics	Haijakidhi
Ndengaro Company Limited	Haijakidhi
Jonz Express Logistics And Supplies Limited	Haijakidhi
Cmtl Group Limited	Haijakidhi
Marathon Logistics Limited	Haijakidhi
Geamos Company Limited	Haijakidhi
Easy Movers And Shipping Limited	Haijakidhi

### Jedwali 3.5a Ubora wa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kanda A (88% ya bidhaa zipokelewe ndani ya siku tatu (D+3))

Mtoa huduma ya usafirishaji wa vifurushi na vipeto ndani ya nchi	Kasi ya uwasilishaji kwa eneo la kanda B (D+3(88%))
Ellymo Company Limited	Imekidhi
Blaze Concierge And Courier Services Limited	Imekidhi
Marathon Logistics Limited	Imekidhi
Simba Logistic Equipment Supply Co. Ltd	Imekidhi
Sga Cash In Transit (T) Limited	Imekidhi
Segax Group Limited	Imekidhi
Mwanga Logistics And Distribution Ltd	Imekidhi
Geamos Company Limited	Imekidhi
Jonz Express Logistics And Supplies Limited	Imekidhi
Kleafast couriers and logistics	Haijakidhi
Ndengaro Company Limited	Haijakidhi
Easy Movers And Shipping Limited	Haijakidhi
Cmtl Group Limited	Haijakidhi

TCRA imechukua na itaendelea kuchukua hatua stahiki za kiudhibiti kwa watoa huduma wote walioshindwa kukidhi vigezo vilivyoainishwa kwa mujibu wa kanuni husika.

### 3.6 Leseni za huduma ya posta na usafirishaji wa vifurushi na vipeto

Aina ya leseni	Idadi	
	Septemba 2024	Disemba 2024
International Courier	6	6
East Africa Courier	2	2
Intercity Transporters	76	79
Intracity Courier	16	18
Public Postal	1	1
Domestic Courier	47	47

## 4. Hitimisho

Kwa muhtasari, ripoti hii inaeleza maendeleo ya sekta ya mawasiliano kufikia mwezi Desemba 2024. Inaeleza hali ya mabadiliko na mwenendo wa takwimu katika sekta ndogo ya mawasiliano ya simu na Intaneti, Utangazaji na Posta na usafirishaji wa vifurushi kwa kipindi cha robo mwaka kufikia desemba 2024 ikilinganishwa na kipindi cha robo mwaka kufika Septemba 2024. Takwimu hizi ni muhimu kwa ajili ya kupima ukuaji wa sekta na pia kubainisha fursa zinazojitokeza katika sekta ya mawasiliano.

Katika kipindi husika, sekta ya mawasiliano ya simu na intaneti imeonesha ongezeko la kuenea kwa miundombinu na idadi ya watu waliofikiwa na huduma. Watu waliofikiwa na huduma ya 3G walikuwa asilimia 91 na 4G asilimia 88, wakati huo eneo liliofikiwa na huduma ya mawasiliano ya 3G na 4G ilikuwa asilimia 74 na 71 mtawalia. Aidha, upatikanaji wa 5G, ulifikia asilimia 20 ya idadi ya watu.

Idadi ya usajili wa laini za simu na matumizi ya huduma za mawasiliano yaliongezeka kwa kiasi kikubwa katika kipindi hiki. Uwepo wa hali ya ushindani mkubwa baina ya watoa huduma ulisaidia kuongezeka ubunifu na kushuka au kutoongezeka kwa gharama za huduma. Ubunifu wa huduma na bei za ushindani ziliwanufaisha watumiaji kwa kuwapatia chaguo bora na thamani kwa fedha zao katika kutumia huduma za mawasiliano.

Huduma za utangazaji pia zimeonyesha ukuaji, hasa katika upatikanaji wa huduma na ongezeko la idadi ya watumiaji wa huduma. Idadi ya watu waliofikiwa na huduma ya Radio FM ilifikia asilimia 78.3 na idadi ya watu wanaopata huduma ya Televisheni ya kidijitali ya Ardhini (DTT) ilikuwa asilimia 58. Mamlaka ianendelea kuhamasisha ogezeko kwa maudhui ya ndani ili kuhakikisha kuwa huduma za utangazaji zinakidhi mahitaji na mapendeleo mbalimbali ya watu.

Shirika la Posta Tanzania na makampuni za usafirishaji wa nyaraka, vifurushi na vipeto ziliendelea kuwa na nafasi kubwa katika kukuza soko lenye ufanisi na nguvu. Kuboresha ufanisi na uaminifu wa huduma za posta na kampuni za usafirishaji mizigo kwa haraka na uhakika ni muhimu ili kukidhi mahitaji yanayoongezeka ya soko la rejareja kwa njia ya mtandao. Kuongezeka kwa biashara kwa njia ya mtandao kumeleta fursa ya mahitaji ya huduma za usafirishaji wa mizigo majumbani na ofisini. Mamlaka itaendelea kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika kufuatilia huduma za vifurushi ili kukidhi matarajio ya wateja na kuboresha utendaji wa sekta hii ndogo ambayo inachangia kwa kurahishisha upatikanaji wa huduma.

Kwa ujumla, mafanikio yaliyoelezwa katika ripoti hii yanaonyesha mchango mkubwa wa sekta ya mawasiliano katika kukuza uchumi wa kidijitali. Ongezeko la miundombinu ya mawasiliano, upatikanaji wa huduma bora za mawasiliano ya simu na intaneti, pamoja na maendeleo katika utangazaji na huduma za posta, vinaimarisha uwezo wa wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi wa kidijitali. Ushindani na ubunifu katika huduma za mawasiliano umeleta manufaa kwa watumiaji, hususan huduma za fedha mtandao, kufanya biashara mtandao, na kurahisisha upatikanaji wa habari. Uwekezaji endelevu katika teknolojia za kisasa na upanuzi wa huduma za mawasiliano ni hatua muhimu ili kuhakikisha kuwa maendeleo haya yanawanufaisha wananchi kwa ujumla na wote wanashiriki kikamilifu kwenye uchumi wa kidigiti.



Mwasiliano Towers,  
20 Sam Nujoma Road,  
14414 Dar es Salaam, Tanzania.  
Email: dg@tcra.go.tz

 @tcra\_tanzania

